**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 23 Februari, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti**:

Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

23. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali za Mitaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zinatakiwa kutenga fedha katika mapato yao ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo, mabaraza ya vijana na vikundi mbali mbali vya uzalishaji kwa kuwapatia mitaji, vifaa pamoja na elimu katika shughuli zao.

(a) Je, kwa mwaka wa fedha 2020 - 2021, Mabaraza ya Miji na Halmashauri ngapi zimeweza kutenga fedha na vifaa kwa ajili ya vikundi hivyo.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha ambazo kila kikundi kimepatiwa kutoka Mabaraza ya Miji na Halmashauri Unguja na Pemba ikiwa ni kutekeleza agizo hilo la Serikali kusaidia makundi hayo maalum.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

114. MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (Jimbo la Shaurimoyo) Atamuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali imepitisha utaratibu wa kuzifunga Bureau-de change zote za binafsi na kuziachia benki kutoa huduma zote za kubadilisha pesa za kigeni hapa nchini.

Utaratibu huo umesababisha usumbufu kwa wageni na wafanyabiashara wengi hasa wanapokwenda benki huwa wanakosa kupata pesa za nchi tofauti ambapo kwa hivi sasa pesa zinazopatikana ni zile maarufu kama vile Dola, Euro. Pounds, lakini pesa za nchi nyengine ikiwemo, Yuan, Crona na nyengine wakienda kwenye benki huwa wanaambiwa hazipo.

(a) Je, Mhe. Waziri hatuoni kuziondoa hizi Bureau-de change kumesababisha usumbufu mkubwa kwa wageni wanaokuja Zanzibar.

(b) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa wakati umefika wa kuzirudisha Bureau-de change kuendelea kutoa huduma hizo ili kuondoa usumbufu kwa wageni na wafanyabiashara.

(c) Kwa kuwa Bureau-de change zilitoa ajira nyingi kwa vijana wetu wengi hatuoni kuwa maamuzi haya magumu tumepoteza ajira nyingi kwa vijana na wananchi wetu wengi na hapa hatuoni kuwa kuzirejesha Bureau-de change tutarudisha ajira kwa wananchi wetu na kupunguza umaskini.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

137. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Serikali inatambua mchango wa elimu na mafunzo ya madrasa katika jamii yetu, kwani kutasaidia kupatikana kwa maadili mema. Hata hivyo, kutorasimishwa elimu ya madrasa kutapunguza ufanisi na kupelekea kuporomoka kwa maadili.

(a) Je, hatua gani zimechukuliwa na Serikali katika kurasimisha elimu na mafunzo ya madrasa Zanzibar.

(b) Je, ni vigezo gani vinavyotumiwa na Serikali kuruhusu majengo yanayoendesha elimu na mafunzo ya madrasa sambamba na kuzingatia afya za watoto.

(c) Je, ni vigezo gani vya elimu na taaluma pamoja na viwango gani vya malipo vinavyotambulika na Serikali kwa walimu wa madrasa.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

68. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Hivi sasa kuna usumbufu mkubwa katika kituo cha afya Tasaf Tazari. Kituo hiki hakina huduma ya umeme na madaktari ndio walipaji wa umeme huo inapofika mwisho wa mwezi hali inayopelekea wakati mwengine wagonjwa wanaofika kituoni hapo kukosa huduma wanazohitaji. Hata hivyo, kinafahamika wazi kuwa wakati mwengine waheshimiwa husaidiana na madaktari kulipa huduma hiyo ya umeme.

(a) Je, ni nani mwenye dhamana ya kulipa huduma hii.

(b) Je, ni lini huduma hii itarudi kituoni hapo.

123. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kumekuwa na ukosefu wa daktari bingwa “specialist” katika hospitali ya Chake Chake ambapo daktari mmoja aliyekuwepo tayari amepewa uhamisho kwenda Unguja.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wakuleta mbadala wake ukizingatia hospitali ni kubwa na ni muhimu kuwepo na daktari bingwa.

(b) Je, ni lini atapatikana daktari bingwa “specialist” katika hospitali hiyo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

16. MHESHIMIWA NASSOR SALUM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hivi karibuni dunia imeshuhudia mashindano ya Olympic yakifanyika Tokyo, nchini Japani ambako michezo mbali mbali ilishindaniwa nchi kadhaa kupata medali. Hata hivyo, Tanzania haikuwa na washiriki wengi kwa michezo mengine ambayo uwezo wa kushindana tunao mfano, kurusha mkuki, tufe, kulenga shabaha, kunyanyua vitu vizito, kuogelea n.k.

(a) Je, Serikali inao mpango wa kuwekeza kwa vijana wa skuli kuanza kujifunza michezo hiyo ili baadae Tanzania itowe washindani bora katika michezo hiyo badala ya kuwekeza mpira peke yake.

(b) Je, Serikali imefanya utafiti kuhusu manufaa ya kiuchumi na kijamii kuhusu michezo hiyo na kama bado lini utafiti kama huo utafanyika.

(c) Taratibu gani inafanyika ili nchi iweze kupata nafasi ya ushiriki wa michezo hiyo Olympic.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

60. MHESHIMIWA JUMA ALI KHATIB (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Mwaka juzi (2020) transfoma iliyopo baina ya Skuli ya Uweleni na Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani Pemba iliripuka na kuzua taharuki kubwa kwa wagonjwa, wafanyakazi, walimu, wanafunzi pamoja na wakaazi wa maeneo hayo.

(a) Je, ni lini transfoma iliyopo karibu na majengo ya huduma za jamii itabadilishwa na kuwekwa katika eneo jengine lililo salama ili kuepusha madhara.

(b) Je, ni kipindi gani mafundi wa Shirika la Umeme (ZECO) huzikagua transfoma zinazofanya kazi kabla hazijaanza kupata hitilafu na kuleta hasara zaidi kwa wananchi na Shirika lenyewe la ZECO.

(c) Je, Wilaya ya Mkoani ina transfoma ngapi ambazo ni nzima na ngapi ni mbovu.

132. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Shirika la Umeme "ZECO" kwa usambazaji wa umeme katika vijiji mbali mbali Unguja na Pemba, lakini katika shehia ya Mwambe na Mchakwe tunavyo baadhi ya vijiji ambavyo bado umeme haujafika kama vile Kwareni, Kwapesa na Kwakobe.

(a) Je, Mhe. Waziri vijiji hivi unavifahamu.

(b) Je, ni lini vijiji hivi vitapatiwa huduma za umeme.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

110. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwa kuwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2015/2016 imemripoti mwekezaji wa Kiwanda cha Sukari Mahonda kuwa anadaiwa kodi ya ardhi yenye thamani ya Dola za Kimarekani 2,629,998 kwa maeneo mbali mbali aliyokodi. Na kwa kuwa Kamati ya PAC ya Baraza la Wawakilishi kwenye Ripoti yake ya mwezi wa Februari, 2019 iliitaka Kamisheni ya Ardhi kwa kushirikiana na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kufuatilia malipo ya kodi hiyo.

(a) Je, hadi hivi sasa Kiwanda cha Sukari Mahonda kimekamilisha deni lake hilo.

(b) Kama deni hilo bado lipo, Serikali ina mpango gani juu ya Mwekezaji huyo.

149. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikitoa miongozo inayoeleweka kuhusu mamlaka husika za kupima na kugawa ardhi zikiwemo eka. Hata hivyo, katika shehia ya Mzambarauni ndani ya jimbo la Pandani kumekuwa na uvunjifu wa sheria ambapo Sheha amekuwa akichukua mamlaka ya kupima eka huku akijumuisha sehemu za mashamba na ardhi za watu na kuamrisha zichukuliwe na watu wengine wasio halali.

(a) Je, ni upi muongozo wa sasa kuhusu upimaji na ugawaji wa ardhi za eka.

(b) Je, katika shehia ya Mzambarauni, kuna eneo kiasi gani la eka na ongezeko la kiasi gani la ardhi ya eka kwa mwaka 2020/2021.

(c) Je, Serikali inawasaidiaje wananchi ambao ardhi zao binafsi zimejumuishwa kuwa ardhi za eka na kunyang'anywa wakapewa watu wengine.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

38. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada mbali mbali ikiwemo ujenzi wa barabara za kiwango cha lami. Licha ya jitahada hizo kumekuwa na tishio la ongezeko la viashiria vya kutokea ajali katika maeneo mbali mbali hapa Zanzibar.

(a) Je, ni lini Serikali itaweka alama katika barabara za Micheweni hasa katika eneo la skuli ya sekondari ya Dkt. Amani Karume, skuli ya Micheweni karibu na kituo cha Micheweni, Kiuyu Mbuyuni pamoja na skuli ya msingi Maziwa Ng'ombe.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimepangwa kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022 kwa utekelezaji katika kukabiliana na changamoto hii.

44. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIR (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika kuendeleza kauli ya Serikali ya kudai risiti wakati wa kutumia pesa, kuna eneo muhimu sana halina risiti nalo ni gari za abiria.

Je, ni lini Serikali itaandaa mpango mzuri kwa gari za abiria kutoa risiti.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

98. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika Mkutano wa Nne wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda aliliahidi Baraza hili Tukufu kuwa, jengo la Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) liliopo Chake Chake, litajengwa kuanzia mwezi wa Septemba mwaka 2021. Hata hivyo, hadi leo hii, jengo hilo bado halijajengwa

(a) Je, kuna sababu gani mpaka leo zilizopelekea jengo la ZSTC kutokujengwa.

(b) Kwa kuwa ahadi ya kujengwa kwa jengo hilo haijatekelezwa hadi leo, Je, kwa nini kitendo cha Mheshimiwa kisizingatiwe kuwa ni cha kulidanganya Baraza.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Elimu:**

93. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Baraza la Mitihani la Zanzibar huwatumia walimu katika kazi za usimamizi na usahihishaji wa mitihani ya Taifa ya Zanzibar.

(a) Walimu wanapomaliza kazi, ni sababu gani hupelekea malipo yao kuchelewa sana.

(b) Ni kwa nini malipo yanayolipwa Unguja yanatafautiana na malipo ya Pemba.

(c) Kwa nini kunakuwa na upungufu wa baadhi ya vifaa mfano magodoro ya kulala.

130. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika malengo ya mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni kujenga skuli tatu za msingi katika maeneo ya Kidichi, Nanguji na Pujini.

(a) Je, Mhe. Waziri unalifahamu lengo hili.

(b) Je, ni lini ujenzi huo utaanza katika sehemu hizo.

## III. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:**

Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**23 Februari, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**